

Maneno yako ni roho na uzima

(Zab. 18,8,9,10,15.)

M.: Maitre Daniel RUGAMIKA BAKULIKIRA.



K/ Ma-ne - no ya - ko, e - e Bwa - na, ni ro-ho na u - zi - ma.



1. Sheria ya Bwana ni kamilifu,
yatuliza roho;
Mafundisho ya Bwana ni imara,
yamletea mjinga elimu.
2. Amri za Bwana ni za haki,
Zafurahisha moyo,
agizo la Bwana ni safi,
layatia macho mwangaza.
3. Ibada kwa Bwana ni safi,
yadumu hata milele;
hukumu za Bwana ni kweli,
zote za haki kamili.
4. Maneno ya kinywa changu yakupendeze wewe,
nayo mawazo ya moyo wangu
yaliyo mbele yako, ee Bwana,
Mwamba wangu na Mkombozi wangu.